Research Journal in Modern Languages and Literatures
https://royalliteglobal.com/languages-and-literatures

Languages & Literatures

Review Article

Section: Literature, Languages and Criticism

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 5th April 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# The philosophy of Wanyore metaphor: A semantic approach

**Henry Andele**[1], **Susan Choge**[2], **Fred Wanjala**[3]
[1] Masinde Muliro University of Science and Technology, Kenya
[2] Koitaleel Samoei University College, Kenya
[3] Kibabii University, Kenya
Correspondence: andelehenry@yahoo.gmail.com

**Abstract**

This paper sought to analyse the philosophy of metaphor in the Banyore proverbs. The paper identified different types of metaphors in the Banyore proverbs and evaluated the metaphor philosophy in the proverbs. This was guided by Relevance: Communication and Cognitive Theory, founded by Sperber and Wilson (2004 & 1986). The Relevance: Communication and Cognitive Theory by Sperber and Wilson (1986) was used to analyse, explain and interpret philosophy and meaning of metaphors in the Banyore proverbs. The study population was conducted on the Banyore natives of Emuhaya and Luanda sub-counties in Vihiga County. Purposive sampling was used to get the Banyore natives who speak the Banyore language and who are fully conversant with the Banyore proverbs. Data collection was done through content analysis and interview. Research instruments included interview schedules and questionnaires. The proverbs were recorded, translated and interpreted in Kiswahili. The research findings established that Banyore proverbs are rich in various philosophies such as forgiveness and reconciliation of the society, marriage and family life. The importance of research findings include documentation of the Banyore proverbs which are rich in their philosophical meaning.

**Keywords:** metaphor, proverbs, philosophy, society, semantic

**Public Interest Statement**

Banyore proverbs are rich in various philosophies such as forgiveness and reconciliation which can be used to enhance cohesiveness in marriage and family life.

**How to Cite:**
Andele, H., Choge, S., & Wanjala, F. (2021). The philosophy of Wanyore metaphor: A semantic approach. Research Journal in Modern Languages and Literatures, 2(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/languages-and-literatures/article/view/584

© 2021 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Research Journal in Modern Languages and Literatures
Volume 1 Issue 2 ISSN: 2709-4316

Review Article

Section: Literature, Languages and Criticism

Check for updates

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 5th April 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# Falsafa ya jazanda katika methali za jamii ya Wanyore: Mtazamo wa kisemantiki

**Henry Andele**[1], **Susan Choge**[2], **Fred Wanjala**[3]
1 Masinde Muliro University of Science and Technology, Kenya
[2] Koitaleel Samoei University College, Kenya
[3] Kibabii University, Kenya
Correspondence: andelehenry@yahoo.gmail.com

**Ikisiri**

Makala hii inatokana na utafiti ambao uliazimia kutathmini falsafa ya jazanda katika methali za Wanyore kwa mtazamo wa kisemantiki. Madhumuni ya makala yenyewe yanahusu falsafa ya msamaha na maridhiano ya kijamii, unyumba na maisha katika ndoa na uadui katika methali za Wanyore. Nadharia ya Uhusiano ya Sperber na Wilson (2004 & 1986) ndiyo iliyoongozwa makala hii. Nadharia hii ilitumiwa kufafanulia maana za methali katika jamii ya Wanyore. Data ilikusanywa kutoka kwa Wanyore wanaoishi katika kaunti ndogo ya Emuhaya na Luanda katika kaunti ya Vihiga. Makala hii ilitumia njia za uchanganuzi matini na mahojiano kukusanya data. Vifaa vilivyotumiwa vilikuwa ratiba ya usaili na tepurekoda. Data ilichanganuliwa kimaelezo kwa kunukuu methali za Kinyore, kisha zikatafsiriwa na kufasiriwa katika Kiswahili hatimaye falsafa ya jazanda ya msamaha na maridhiano ya kijamii na uadui ikaainishwa na kufafanuliwa. Matokeo ya kazi hii yatachangia kueleweka kwa falsafa ya jazanda ya msamaha na maridhiano miongoni mwa wanajamii. Pia, yatakuwa mchango na marejeleo kwa watafiti katika uwanja wa methali.

**Maneno muhimu:** falsafa, jazanda, jamii, methali, semantiki,

## How to Cite:
Andele, H., Choge, S., & Wanjala, F. (2021). The philosophy of Wanyore metaphor: A semantic approach. Research Journal in Modern Languages and Literatures, 2(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/languages-and-literatures/article/view/584

## Utangulizi

Methali ni semi au kauli teule zinazotumiwa na watu katika uelekezaji, ubainishaji na uwasilishaji wa masuala muhimu ya jamii. Katika mapokeo ya jamii methali zimetumiwa kama vielelezo vya hisia, itikadi, maono na pia katika ubainishaji kwa utaratibu kuhusu maisha ya watu (Masolo, 1994). Hivyo basi, methali ni zao halisi la jamii na kanzi mojawapo katika uhifadhi na uwasilishaji wa tamaduni za jamii. Kila jamii ina methali zake ambazo huwa nembo ya kutambulisha kikundi cha watu. Ujumbe katika methali huweza kufasiriwa kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kwa mafumbo, kutokana na ruwaza ya tamathali za semi zinazotokana na mazingira ya jamii husika (Maitaria & Momanyi, 2016). Katika mawasiliano ya jamii, methali husaidia kubainisha fikra za watu kuhusu mafikira ya kiulimwengu kwa njia ambayo inaafiki malengo, matakwa na matarajio yao katika jamii (Maitaria, 2020). Yaani, methali katika jamii ya Wanyore ni kielelezo na vipumuzi vya utamaduni wa watu. Licha ya kutilia podo mazungumzo, methali za Wanyore ni chombo au kifaa cha kubainishia falsafa ya Wanyore kwa kuzingatia tajriba na uhalisia wa maisha ya watu katika miktadha ya kihistoria ya jamii. Basi methali zinapotumiwa kubainika katika muktadha ambamo zimetumika, huibua na huielekeza mijadala ambayo ina azma ya kufikia maamuzi fulani kuhusu maswala yanayowahusu watu katika jamii hiyo.

Hekima au busara ndicho kiini au maana iliyofutikwa katika methali. Methali nzuri kwa kawaida inamaana zaidi ya moja kwa sababu hekima iliyo ndani yake inapasa kusadifu miktadha ya aina mbalimbali kulingana na haja ya mtumiaji. Maana ya methali yaweza kukidhi mahitaji ya mtumiaji kwa namna yake kadri ya mazingira na wakati wake lakini bado hekima ya methali hiyo itaendelea kuwa aushi hata kwa mazingira na nyakati nyingine tofauti. Ni kutokana na sababu hii uchambuzi wa maana ya methali unaweza kufanyika katika ngazi tatu ambazo ni za muhimu ili kuifasili kwa usahihi. Ngazi ya kwanza huzingatia maana ya maneno yaliyotumika na kulinganisha maana hizo na ukweli wa maneno hayo. Ngazi ya pili huzingatia mshabaha wa maana ya ngazi ya kwanza na kuifasili kwa ndani ili kuivika maana pana na ya jumla zaidi. Hatimaye, ngazi ya tatu huzungatia lengo la mzungumzaji kwa mujibu wa muktadha, mazingira au hali inayozungumziwa wakati huo. Katika hatua hii, kila moja ya sehemu au hali zinazoelezeka katika methali yenyewe huchukua maana tofauti kulingana na mahitaji na mtumiaji.

## Mapitio ya Maandishi

Kwa mujibu wa Culler (2001) na White (1984) jazanda ni jumla ya maono ya akili ambayo ni yenye uelewa au uchukulio wa juu wa kimawazo. Naye Mbatiah (2001) anaieleza jazanda kuwa ni kunga ya utunzi inayotumia lugha kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi. Imbosa (1990) alihakiki jazanda zilizotumika katika baadhi ya mashairi ya Muyaka bin Haji. Aliifasili jazanda kuwa ni mojawapo ya mbinu za uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili. Alionelea kwamba matumizi ya jazanda yanapaswa kuchanganuliwa na kufafanuliwa ili hadhira lengwa ifahamishwe kuhusu uhalisi wa maisha unaoakisiwa, uumbuji wa sanaa iliyotumika na utamaduni wa jamii inayohusika. Imbosa alizingatia maneno teule yaliyotumika kujengea jazanda, kuibulia hisi na uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Isitoshe, methali ni njia

ya uwasilishaji wa maudhui kuhusu masuala mbalimbali yanayoizungukia jamii.

Maitaria (1991) anaiona jazanda kuwa ndiyo kiini cha maana ya methali fulani - hasa maana ya ndani iliyofichama. Jazanda hiyo huhitaji kufafanuliwa ili kupata maana kamili katika muktadha wa kijamii unaohusika. Jazanda inayosawiriwa aghalabu huwa haina uhusiano wa moja kwa moja na maana ya maneno yanayoiunda tungo ya methali inayohusika.

Akifuatia Chacha (1987) aliyechunguza usawiri wa jazanda katika ushairi wa Kiswahili, Maitaria (2012) anashikilia kwamba jazanda katika tungo za kishairi hufafanuliwa vyema kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni na uhalisia wa maisha ya jamii inayohusika. Kwake, mshairi huibua jazanda kutokana na tajriba yake katika jamii. Maudhui ya methali husawiriwa na kuwasilishwa kutokana na jinsi jazanda zilivyojengwa. Ujumbe unaowasilishwa katika jazanda zilizomo kwenye tungo za methali pia hupata ufasiri wake kwa kuzingatia vipengele vya muktadha, tajiriba na utamaduni wa jamii inayohusika. Pamoja na kwamba tafiti za Chacha na Maitaria zilihusu uchambuzi wa jazanda katika ushairi wa Kiswahili, ziliofaidi utafiti huu kwa namna ambavyo nao ulitathmini falsafa ya jazanda katika methali za jamii ya Wanyore kwa mtazamo wa kisemantiki. Matumizi ya methali katika jamii husawiri itikadi, uzoefu, uhalisia na mielekeo ya jamii ya Wanyore.

Kwa mujibu wa vijelezi vilivyohakikiwa, methali za jamii fulani hufungamanishwa na dhana maalumu ambazo ni zao la mazingira na miktadha ya kitamaduni na kijiografia. Kupitia kwa methali, mila, desturi, mali, amali na utamaduni huwasilishwa na kuhifadhiwa. Maana iliyoghubikwa kwenye methali hizo huweza kufasiriwa kikamilifu kwa kuhusisha utamaduni na miktadha ya kijamii na kijiografia ambamo methali hizo hutumika. Iwapo hadhira inayolengwa itaufasiri ujumbe unaohusika nje ya miktadha ya utamaduni na eneo linalohusika, ujumbe huo utapotoka au maana iliyokusudiwa kupotea.

Kama ilivyo kwa ushairi (Maitaria, 2012; Imbosa, 1990; Abdalla, 1973 na Noor, 1988), maana ya methali hufasiriwa na kufumbuliwa kwa mujibu wa miktadha ya kijamii inayohusika. Ufafanuzi wa methali huhitajika ili maana na matumizi yake yabainishwe. Maana ya methali aghalabu husitiriwa katika jazanda zinazohitaji kufumbuliwa na kuelezwa ili zifahamike. Methali zilizopambwa kwa jazanda zinazosawiri mazingira na miktadha mahususi ya kijamii aghalabu huwa kichocheo cha tafakuri kuhusu kadhia zinazowasibu wanajamii wanaohusika. Waaidha, ni kutokana na jazanda, ishara na taswira mbalimbali zilizotumika katika methali ambapo dhana, maana au ujumbe uliofichama humo kuhusu masuala nyeti katika jamii hufichuliwa na kufafanuliwa.

Parker (1970) anashikilia kwamba maana na fasiri ya methali yoyote ile haina budi kuambatana na utamaduni wa jamii inayohusika. Naye Msuya (1977) analiendeleza wazo hilo kwa kueleza kwamba kutokana na methali tunaweza kuipata taswira au hisi ya utamaduni wa wanajamii wanaohusika. Yaani, methali huwa mwangwi wa maisha na mazingira ya jamii inayohusika. Kwa upande wake, Saville-Troike (2003) haonyeshi tofauti kubwa na mawazo ya Parker anaposema kuwa lugha na utamaduni ni kama sarafu kwa ya pili.

Methali hutumia tamathali anuwai za usemi. Methali pia hulinganisha hali mbili tofauti; msingi unaaowezesha methali kulinganisha na kuzipatanisha hali mbili tofauti ni

ile sifa kwamba kila methali ina ustiari wa kiwango fulani ndani yake. Ustiari huo huzipima pande mbili na kuzilinganisha kwa jambo ambalo zote zinalichangia. Uchambuzi wa istiari za methali hutokana na jinsi tamathali zilivyotumika. Kwa ujumla, methali husheheni matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbiha, istiari zinazohusu mwenendo wa binadamu, balagha iliyochanganywa na chuku, kejeli, vidokezo vya matukio halisi, pamoja na uzingatiaji wa mienendo, maumbile au tabia za vitu katika maisha ya kila siku.

Akichunguza jazanda katika methali za Kihaya, Seitel (1972) alisisitiza kwamba methali yoyote hupata maana kutokana na vile jazanda ilivyotumika. Alishikilia kuwa methali nyingi huwa na uhusiano mkubwa na utamaduni wa jamii inayohusika. Maana iliyokusudiwa na methali fulani mara nyingi hufafanuliwa kwa kuzingatia jamii inayohusika. Utafiti huu ulinufaika kutokana na maelezo ya Seitel kwamba methali hufafanuliwa kwa namna mbili muhimu: ufafanuzi unaozingatia maana ya juu juu na ufafanuzi unaozamia ndani zaidi ili kupata maana fiche. Fauka ya hayo, Seitel alieleza kwamba maana inayokusudiwa katika methali ni ile fiche na ambayo hubainika baada ya kuchambua jazanda iliyomo katika methali inayohusika. Hata hivyo, utafiti wetu ulichukulia kuwa methali za jamii ya Wanyore zina jazanda ambazo husheheni falsafa ya Wanyore. Kwa hali hiyo, utamaduni, mila na itikadi zao zimekitwa katika falsafa yao. Ili uweze kuelewa maana ya jazanda hizo sharti ujikite katika mazingira ambamo methali hizo zimetungiwa. Hivyo ni kusema kwamba methali hizi huwasilisha ujumbe fulani kwa mujibu wa muktadha maalumu.

Utafiti wetu ulifaidi mbinu za utafiti pamoja na misingi ya Mtesigwa (2013) aliyechunguza matumizi ya methali katika nyanja za ndoa, malezi, kazi, ushujaa, umoja na ushirikiano katika maisha ya nadharia ya Sperber & Wilson. Ingawa maadili ni sehemu ya falsafa, mtesigwa alichunguza maana na matumizi ya methali katika mazingira na jamii tofauti na ile ya Wanyore inayochunguzwa. Aidha, alizamia muundo na dhima ya methali katika jumuiya lugha kwa ujumla wake.

Imebainika kwamba fanani anapotumia methali katika miktadha mbalimbali ya kijamii huwa hashurutishwi kuzifafanua. Haelezi maana wala matumizi ya methali hiyo katika jamii, bali hutumia maneno machache teule kuwasilisha ujumbe wake kwa walengwa. Ufafanuzi mwingine huachiwa hadhira yenyewe kujifafanulia au kujijazia. Kwa hivyo, pasipokuwepo uelewa wa kina kuhusu methali na namna zinavyotumika kwenye miktadha ya kijamii, huenda maana na dhana potovu zikaibuka. Kuna haja ya kuzifafanua jazanda zilizotumika katika methali za jamii mbalimbali za Kiafrika. Jazanda hizo ndizo zinazositiri falsafa za jamii zinazohusika.

## Kijelezi cha Jazanda

Kwa ujumla wa fasili yake, jazanda ni kunga ya utunzi inayotumia lugha kusawiri taswira fulani kutokana na ufafanuzi unaotumia msamiati au tamathali teule za usemi. Jazanda humwezesha msikilizaji kuona, kuonja au hata kuhisi kitu kinachoelezwa. Jazanda huhusisha ulinganishaji wa vitu viwili moja kwa moja bila kutumia vifananishi au vilinganishi. Kitu au neno hupewa sifa na maana batini au isiyo ya kawaida. Jazanda hutumiwa kukolezea utamu, msisitizo na mvuto wa kisanaa katika lugha inayohusika. Mvuto huo ndio huifanya lugha ya kifasihi kuwa na mnato na ufasaha zaidi ikilinganishwa na nyanja nyingine za matumizi ya

lugha. Vivyo hivyo, azma ya mtumiaji wa methali huwa ni kuifumba maana yake.

**Njia za Ukusanyaji Data**

Utafiti ulishirikisha Wanyore ambao ni wazawa na wazungumzaji wa lugha ya Kinyore wanaopatikana katika kaunti ndogo za Emuhaya na Luanda ambao waliteuliwa kimaksudi. Uteuzi wa kiupokezano ulitumiwa kuwafikia watu walio na umilisi mkuu katika methali za Kinyore na falsafa yake ambao ni nadra kupatikana. Kwa njia hii, Mmilisi wa kwanza kufikiwa aliombwa kuelekeza mtafiti kwenye wale wengine kama wao hadi wakafikia 17. Uteuzi faafu ulitumiwa kuteua na kushirikisha washiriki wote waliopatikana katika shughuli halisi za kiutendaji katika jamii kama vile: mabaraza ya machifu na manaibu wao, harusi na matanga.

**Nadharia ya Uhusiano**

Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986) na wakaiendeleza (2004) ndiyo iliutesi, kukosana au dhuluma. Matumizi ni kuwa iwapo mtu anachokoza au kuudhi wenzake pia kuna wakati ambapo naye atatuhumiwa. Ni jambo la busara kuchunguza na kubaini asili ya yoongoza utafiti huu. Nadharia hii ilitumiwa kufafanulia maana za methali katika jamii ya Wanyore. Kadhalika, ilitumiwa kueleza na kufasili hali za kimawasiliano katika methali za Wanyore. Nadharia hii ilitumika kufafanua maana kiisimu kupitia uchakataji na kuitajirisha katika kiwango cha kipragmantiki hadi maana itakayopatikana ihitimishe kiwango cha uhusiano unaohitajika. Kwa mujibu wa nadharia hii ufasiri wa maana iliyosimbwa katika jazanda ambayo si dhahiri huwekwa wazi ili kuona uhusiano unaotarajiwa. Hii nadharia katika mhimili wake mkuu wa uhusiano na ufasiri wa jazanda ni mawasiliano ambapo maana fiche zaidi ya ile ya kawaida sharti ifikiwe kwa kufuata sifa za vitu viwili; maana ya kisemantiki na maana ya kipragmantiki. Usemi wa methali huwasilishwa na ishara ambayo mzawa wa lugha hiyo au msikilizaji huielewa kwa kusaidiwa na muundo na mfumo wa lugha, ili kuelewa maana kisemantiki katika usemi huo. Falsafa ya methali ilibainika katika muktadha wa kimatumizi.

**Falsafa ya Msamaha na Maridhiano ya Kijamii**

Katika jamii ya Wanyore, zipo methali ambazo zinasisitiza msamaha na maridhiano kama njia ya kuleta wema na uhusiano mzuri. Methali hizi aidha hutaja ubaya ambao ukimfanyia mtu au wenzako pia nawe utafanyiwa. Vilevile hufafanua kuwa ikiwa umetendewa ubaya sharti uweze kusamehe na kuendelea na maisha. Kwani maridhiano ya wanajamii ni bora na huendeleza amani na upendo miongoni mwa watu. Wanajamii waishi kwa kushirikiana katika mambo yao, yawe mepesi au magumu. Kupitia falsafa hii ni kuwa wanajamii Wanyore wanahitajiana kwa kila jamii. Methali hizi zinadhihisha kuwa hata mtu awe na uwezo mkubwa au tajiri kuna wakati au siku ambayo atahitaji wale ambayo ni masikini au wenye uwezo mdogo. Basi haja kubwa ya kuwa na msamaha na maridhiano na kila mtu katika jamii.

Falsafa hii imejitokeza katika methali nambari ya 1, 2, na 3.

1. Omurindi arindilwanga (Tafsiri: Mchokozi huchokozwa)

Jazanda ipo katika neno "omurindi" kwa maana ya mchokozi, mtu anayeudhi au anayechokoza wenzake au anayejitetea. "Arindilwanga" ni kuchokozwa lakini maana yake ni kudhulumiwa. Maana ni kuwa mtu mchokozi naye pia atachokozwa. Muktadha hutumika katika hali ya kitendo cha mtu kabla ya kumhukumu. Iwapo mtu amejitetea dhidi ya maonevu si vyema kumlaani, bali yule aliyeanza ugomvi ndiye anapaswa kukemewa na kusutwa. Tukiwalaumu wanaojitetea tutakuwa tunaendeleza maonevu na ukiukaji wa haki za watu wanyonge. Palipo na ukandamizaji wa watu, chuki na hiana hutawala na kukwamiza maendeleo. Jamii iliheshimu sana hali ya watu kuishi pamoja pasipo na mizozano.

2. Amayia ketsulisia amakhulu (Tafsiri: Mapya hukumbusha yaliyopita)

Jazanda iko katika "amayia" ni mapya ni mambo yanayotendeka hivi punde. "amakhulu" ni yaliyopita kwa maana ya mambo yaliyotendeka kitambo. Maana ni mambo mabaya yatendwayo sasa hufanya watu waliosameheana kurudia uadui kwa kuwakumbusha yaliyotendeka ya kale.

Muktadha ni wa maridhiano au kutibuka kwa maridhiano, amani au kuzuia vita na ugomvi. Matumizi ni kwamba si vyema kurudia maovu hasaa kimakusudi kwani hali hii hufufua uhasama uliosha.

Katika methali hii wanajamii walihimizwa kuhakikisha kwamba wanajiepusha na mambo ambayo yanaweza kuwatatiza hasaa kwa kukumbuka maovu yaliyopita. Jamii ilisisitiza maridhiano ikiwa kungeweza kutokea hali yeyote ambayo ingezua sintofahamu miongoni mwa watu ikiwa ni kujaribu kuziba mianya yote ambayo ingesababisha uhasama kwa wanajamii. Kwa vyovyote vile, wanajamii hawakupenda kurudi katika hali ambayo iliwakwaza hapo awali. Wanajamii walio na ni muhimu kudumisha au kuganga yajayo ili kuepukana na ya kale ambayo hayana maana kwa jamii kisasa.

3. Mbolelwa semalanga amahofu tawe (Tafsiri: Kuambiwa hakumalizi hamu ya kuona)

Jazanda inapatikana katika neno "semalanga" kwa Kiswahili ni kutomaliza maana iliyondani yake ni kutotegemewa. Maana ya methali kwamba kuambiwa na kuona ni mambo mawili tofauti kabisa. Muktadha ni wa kesi au kutofautiana. Matumizi ni kuwa ili kupata ukweli wa hali au jambo fulani hususan watu wanapokosana ni sharti kutegemea kilichoonekana au kusikiliza pande zote mbili sio kutegemea yale ambayo umeambiwa au kuelezwa tu hasa ya upande mmoja. Waweza kuambiwa masuala ya uongo na ukatoa uamuzi usiofaa. Jambo la kuambiwa halimalizi uchu wa kuona, kuona si kuambiwa. Maridhiano kwa walioteta awali ili kupata suluhu au hukumu ya haki, anayetatua anahitaji kutegemea yaliyoonekana si yaliyozungumzwa au yaliyosemwa ili kupatanisha mahasimu hao. Uamuzi usiegemee upande wowote.

Falsafa ya jazanda inayojitokeza katika methali hizi ni kuwa watu wanapotagusana hasa katika familia au jamii hali ya kutoelewana inaweza kutokea. Muhimu kunahitajika kusameheana na kuridhiana. Watu wakitofautiana maendeleo hukwama. Ili kufanikisha msamaha na maridhiano pande zote zinahitajika kusikilizwa; mlalamishi na mshtakiwa au mshukiwa. Uamuzi ufanywe kwa kurejelea mashahidi si kwamba yatategemea yaliyofanyika awali. Kuambiwa na kuona ni mambao mawili tofauti katika jamii. Wanaofaa kutoa ushahidi

ni wale walioona wala si waliosikia. Uamuzi unaoegemea kwenye mashahidi una ukweli unaoridhisha wahusika wa pande zote. Uamuzi unaoegemea upande mmoja ulichochea vurugu na uhasama zaidi. Badala ya kuwa na maridhiano unaendeleza uadui miongoni mwa wanajamii. Mtazamo wa jamii ulikuwa lazima pawe na msamaha na maridhiano kwa wanaozozana ili kufanikisha maendeleo. Waliokataa kusameheana walichukuliwa kama maadui wa maendeleo ilhali walioridhiana na kusameheana waliepuka kurudia makosa yale yale kwani hali hii huzua uhasama.

**Falsafa ya Uadui na Uhasama**

Katika methali 4, 5, 6 na 7 falsafa ya jazanda ya uadui au uhasama katika methali za Wanyore imejitokeza:

4. Omulembe kwera oukalile (Tafsiri: Salamu zilimuua zuzu au anayezubaa)

Jazanda hapa ipo katika neno "omulembe" ambayo ni salamu, maana ya ndani iliyofichama katika neno hili ni mbinu ya kuficha uhasama. Maana hapa kuwa hata adui au hasimu anaweza kukusalimia, haimaanishi ni rafiki yako. Basi kupitia msamiati huu ni kwamba wakati ambapo hali inatulia, inaonekana kuna amani, inaweza kuwa bandia. Huo ndio wakati mtu anahitajika kuwa mwangalifu zaidi la sivyo anaweza kujikuta pabaya. Muktadha ni wa hadaa za maadui au unafiki. Matumizi ni kwamba. Salamu haimaanishi amani kati ya mahasimu

5. Ingwe yali isilu nebolelwa setilanga ebilenje tawe, etile omundu likosi. (Tafsiri: Chui alikuwa mjinga, alikuwa amemshika mwanadamu miguu lakini akaambiwa awe akishika shingo ili amuue haraka.)

Jazanda ipo katika neno "ingwe" kwa kurejelea chui maana ya ndani ni adui au hasimu. "Omundu" kwa Kiswahili ni mtu lakini maana yake ya ndani ni windo. "etile omundu likosi" ni kukaba shingo hapa inarejelea kuangamiza. Maana ni kuwa usifunze adui maarifa atayatumia kukuangamiza. Ni adui asiyeaminika kiasi cha kumtobolea siri za kukuangamiza, atazitumia kukumaliza. Usimwambie mambo yako ya ndani ni hatari kwa maisha au ufanisi wako. Muktadha ni wa uhusiano hasi au wa utata au uadui au uhasama miongoni mwa wanajamii.

Matumizi ni kwamba adui ni adui usimwamini kiasi cha kumwerevusha. Walio na uadui au chuki dhidi ya wengine hawaachi hulka hiyo licha ya maridhiano au masikilizano yanayofanywa baadaye. Kwa nje wanaonyesha uhasama haupo lakini ndani kwa ndani uadui haukomi. Kwa mantiki hayo, adui usimwamini ama asiaminiwe kwa kiwango cha kumwambia siri za ndani zako. Kuna uwezekano wa kutumia siri hizo kukudhuru.

6. Nolasa lichina muchinzukhi nitsikulasa (Tafsiri: Ukiwashambulia nyuki watakushambulia pia)

Jazanda imejikita katika neno "muchinzukhi" kwa Kiswahili ni nyuki ambapo ina maanisha kuwa watu katika shughuli zao. Maana ni kuwa mtu akiwa na shughuli zake, asiyejihusisha na mambo hayo, asimchokoze au asiingilie maisha yake ya mwenzake ambayo hayamhusu kamwe.

Muktadha ni wa kuchunguza watu kwa mambo yasiyokuhusu wala kukuathiri. Matumizi ni kwamba tusiyaingilie mambo ambayo hayatuhusu tusipatwe na masika

tusiyoyatarajia.

7. Injila yolondanga khwo seli eyokabukhilangakho tawe (Tafsiri: Njia unayofuatia si ili unayotumia wakiti wa kurejea.)

Jazanda ipo katka neno "injila" kwa Kiswahili ni njia hapa jazanda ni mipango ya kibinafsi au siri ya maisha ya kibinafsi. Maana ni kuwa usiyaweke bayana maisha yako ya kibinafsi, unaweza kufahamika kwa urahisi. Muktadha ni wa maisha ya kibinafsi au mipango ya kibinafsi. Matumizi ni kuwa haifai kila mtu kujua utaratibu wa maisha yako, jinsi ambavyo unatekeleza masuala yako ni siri, mahasidi watapata njia rahisi ya kukuponya au hata kukuibia mali yako au itakuwa rahisi kwa maadui zako kukuangamiza.

Falsafa hapa ni kuwa zama za kale, uadui katika jamii tofauti tofauti ulishamiri kutokana na sababu mbalimbali kama vile kung'ang'ania mashamba, maji na wizi wa mifugo. Kwa mantiki hayo haikuwa jambo la busara kumwamini adui kiasi cha kumwerevusha au kumpa siri za jamii yenu. Uhasama ukirudi atatumia maarifa uliompa kukuangamiza.

**Falsafa ya Unyumba na Maisha katika Ndoa**

Falsafa hii imejidhihirisha katika methali ya 8, 9, 10 na 11

8. Owakhwa mao niye soo (Tafsiri: Aliyelipa mahari ya mamako ndiye babako)

Jazanda hapa inajitokeza katika maneno: "owakhwa" ambalo ni kulipa mahari kwa maana kuwa kugharamia unachothamini au kitu cha thamani. Neno "so" ni baba kwa maana ya kuwa aliye na mamlaka au aliye na kauli ya mwisho auanayewajibikia malezi yako. Nalo neno "mao" lina maana kuwa mamako ni kichocheo cha uzalishaji. Maana hapa ni kwamba ukigharamia chochote, una haki ya kufaidika nacho, una haki kupata mavuno yake. Aidha una mamlaka juu yake. Katika ndoa za kitamaduni na hata sasa katika jamii ya Wanyore mahari ni kungo muhimu sana katika kudumisha udhabiti wa wanandoa. Mpwito wa wakati na ujio wa dini za kigeni haujabadilisha dhana ya mahari katika ndoa za kitamaduni za Wanyore. Muktadha ni wa unyumba au ndoa za kitamaduni au umuhimu wa mahari.

Matumiza kulipa mahari na kutunza watoto. Kitamaduni unaweza kuoa mke na ukapewa kibali cha kuwa baba ya watoto wa huyo mke kwa kulipa mahari endapo hukulipiwa mahari. Falsafa ya jamii ni kwamba ili uweze kutoa madai kwamba unamiliki kitu chochote i ni kwa kuwasuta wasiopenda kuvitolea vitu jasho ilhali wanataka kufaidika navyo. Wanaotaka kuoa au kuasi ukapera wawe tayari kuwajibika kwa kulipa mahari na kulea watotot pamoja na familia kama viongozi. Yaani, baba si kuzalisha pekee bali ni uwezo wcha thamani sharti uwe uligharimika kukipata. Ni kutokana na hali hii ni kwamba mume aliheshimiwa. Hii ikiwa inadhihirisha kuwa amewajibika katika suala la ndoa.

9. Uwaleka uwamurela ayumbaanga nabacheni (Tafsiri: Anayedharau aliyemuoa huangaika na wageni)

Jazanda hapa inajitokeza katika neno "ayumbanga" ni kuhangaika kwa maana kwamba kushindwa kuwahudumia wageni. Pia, katika neno "nabacheni" ni wageni ni watu wa kuheshimiwa au watu mashuhuri. Maana yake ni kuwa mke anayemdharau mumewe hutatizika anapotembelewa na wageni kutoka kwao. Hawezi kuwahudumia ipasavyo. Muktadha ni wa unyumba; mahusiano kati ya wanandoa Matumizi ni kwamba ukimdharau mumeo au yeyote anayepaswa kuheshimiwa usitarajie usaidizi wake unapokuwa na uhitaji.

Falsafa hapa ni kuwa katika maisha ya unyumba mke na mume wanahitaji kuheshimiana na kuishi pamoja kwa amani. Hali hii itawafanya waishi pamoja kwa njia nzuri na kushughulikia mambo ya unyumba kwa njia nzuri. Ni kuishi kwa maelewano haitaleta mtafaruku na aibu katika ndoa yao.

10. Andacheenda yakhwa mungo (Tafsiri: Asiyetembea mbali hulipa mahari anakotoka au asiyetembea mbali huoa anakotoka au jirani. Au asiyetembea mbali na kwao hulipa mahari kwao au huwa kwao)

Jazanda hapa inajitokeza neno "andachenda" ni kutotembea inarejelea hali ya kutafuta mke na kutojua sehemu au maeneo ya mbali. "Mungo" ni nyumbani hapa inarejelea kuhusika kitendo cha ndoa na mtu wa ukoo wako au kuoa kwao, kupata mke ambaye mnafahamiana au jirani yako. Maana ni kwamba ukitaka kuoa, zuru maeneo ya mbali utampata mke huko. Wanaoishi karibu huchukuliana kama ndugu, ni vyema kuoa mbali kwa minajili ya kudunisha undugu huo. Watu wanaoishi eneo moja huchukuliana kama ndugu na si vyema kuona hata kama hawana uhusiano wa damu. Ni bora kwa waume kwa wanawake wanaotoka mbali kuoana ili kudumisha heshima na mtagusano. Pia, kuoa mke mnayejuana kwa muda mrefu huzua dharau maana tayari anajua familia yenu na udhaifu wenu. Muktadha ni wa ujirani mwema, unyumba, mahusiano na ndoa. Matumizi ni ya kiutamaduni hata jirani yako ni sawa na ndugu yako haifai kuoana. Kwa wanaodhamiria kuoa ni bora kuoa mtu wa mbali. Mahusiano na jirani huwa sawa na ya watu wa ukoo mmoja, si vyema kuanza mahusiano ya ndoa. Hali kadhalika, kudumisha mlahaka wa undugu ni jambo la hekima kutafuta mchumba mbali na kwenu na kulipa mahari kwingineko wala si kwenu. Vile vile kuoa mbali hupanua au hueneza ujamaa na undugu mbali au sehemu nyinginezo hivyo, ongeza mahusiano na kupunguza uhasama. Kuoa mbali huboresha utangamano na kuchochea maendeleo katika jamii kwa mfano kibiashara, kiuchumi na kisiasa. Falsafa hapa ni kuwa katika jamii wanaume walihimizwa wanapofika umri wa kuchumbiana kutafuta mke mbali na nyumbani kwao. Mapenzi kati ya watu wa karibu hayakukubaliwa au kufurahiwa na wanajamii. Pia, hii ilikuwa onyo kali kwa sababu ukiwa hkuutatafuta mpenzi unaweza kuanza kushiriki na watu wa ukoo wako jambo ambalo ni ma inapigiwa mfano kama onyo na funzo kwa wengine ili hali kama hiyo isiwahi tokea tena. Falsafa hii baado inadumishwa katika jamii kwa kuhamasisha wanajamii kuwa wanahitajika kuwa uhusiano mwema ili kuendeleza jamii kwa njia iliyobora sana na ambayo imesimikwa kwa maadili mema katika jamii. Na ili kudumisha hali hii nyakati zile za zama za kale msichana au mvulana alikuwa anachunguzwa kwa karibu mno akibalehe tu, watu wa ukoo wake hasa akina shangazi walihusika sana katika harakati za kutafuta wachumba. Uhusiano wa karibu kamwe haukurusiwa na kwa bahati mbaya aliyeshiriki kitendo cha ndoa na kumpata mtoto walikuwa wanahamishwa kutoka kwa ukoo huo na kupelelekwa mbali kuanzisha ukoo mwingine huko. Isitoshe, hawakukubaliwa kushiriki chochote na ukoo wao wa awali hata kukula pamoja haikurusiwa kabisa. Hii ilikuwa dhambi kubwa.

11. Uutsia owabwe sachelekhwangwa tawe (Tafsiri: Aendae kwao hatumwi)

Jazanda hapa ipo katika neno "owabwe" kwa maana ya mahali anapotoka (kwao) hapa ni kuwa mahali mtu anajiskia huru. Alikozaliwa mwanamke, kwa wakwe. Maana ni kuwa

mtu akiwa kwao au kwake ana uhuru wa kufanya jambo ambalo kwa kawaida ni vigumu kulifanya kwingine. Inarejelea hali ya kumchunga mke. Katika jamii ilichukuliwa kuwa mwanamke ambaye ameoleka ni mtu mzima ambaye anatambua jambo ambalo ni nzuri au mbaya. Kuwa mwaminifu au kutokuwa ilimtegemea yeye mwenyewe. Muktadha ni wa ndoa. Mtumizi ni kuwa watu wanapoolewa huwa kuna tofauti zao. Falsafa hapa ni kuwa katika ndoa kuna hali za kutofautiana. Jamii ilichukulia kwamba hawa ni watu wawili waliokuja pamoja wakiwa wazima na msimamo tofauti lazima idhihirike katika ndoa zao. Hii hafai kuleta uhasama miongoni mwao. Isitoshe, ikiwa hata kuna hali ya kutoaminiana au kushuku mwingne ana jicho la nje hasa mke basi mme hafai kumwekea masharti hasa wakati anapoenda kwao, kumtuma vitu ili arudi haraka ati unajaribu kudhibiti wakati wake au hata kujaribu kumpimia muda. Haya yote kwa mujibu wa falsafa hii ni bure bilashi, hayana mashiko na huwezi kumchunga binadamu kama ilivyo kwa wanyama au mifugo. Kilicho muhimu ni kutafuta njia mbadala ya kusuluhisha hali yoyote ya sintofahamu kati ya wanandoa.

12. Ouralola nyina bukhana mbu papa yafuba tsing'ombe (Tafsiri: Yule ambaye hakumwona mamake ujanani hudai eti babake alitupa ng'ombe)

Jazanda ipo katka neno "yafuba" ni kutupa kwa maana ya kuharibu au kulipa visivyo. "Tsing'ombe" ni ng'ombe kwa maana ya mahari. Maana ni kuwa mambo au vitu hubadilika kulingana na mpwito wa wakati, kila jambo lina mwisho wake. Hakuna hali inayodumu milele. Muktadha ni wa utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto au vijana au mabadiliko maishani. Matumizi ni, wanaolengwa katika methali hii ni watoto wanaowadharau wazazi wao, hasa mama zao. Watoto wakumbuke ujana ni hatua ambayo watu wote hupitia. Wazee wote walipita hatua hii. Katika ujana wao, hao mama zao walikuwa wanapendeza, wenye nyuso zinazong'aa waliokuwa waking'ang'aniwa na wanaume. Wanapokuwa wazee huonekana dhaifu na uso ulionyauka au usiopendeza kwa kiasi wanaonekana kuwa na sura zisizopendeza. Kutokana na hayo, ng'ombe ambao walilipwa kama mahari walitolewa kihalali wala hawakutupwa na baba. Ni hamasisho kwa watoto kuwaheshimu mama zao na wazazi wao kwa ujumla. Watoto wasio na heshima ni tishio kwa usalama wa kijamii na hata taifa kwa ujumla.

Falsafa inayojitokeza kwenye methali hii ni kwamba jamii ya Wanyore ilithamini sana wazazi na kila mtoto alihitajika kumheshimu mzazi wake. Isitoshe, watoto na hata watu wengine walikumbushwa kwamba hakuna hali yoyote ile inayodumu milele. Kila jambo lina mpito wa kiwakati. Kwa hivyo, kila mwana jamii alihitajika kutafakari kuhusu suala nzima pasipo kuwa na mawazo ya kijuujuu au finyu kuhusu hali husika.

Falsafa ya jamii ya Wanyore ilichukulia suala ya mahari kwa uzito. Kila mwana jamii alihitajika kumlipia mkewe mahari. Hii ilikuwa ishara ya heshima na umilikaji. Mahari ilihitajika kulipwa yote kabla ya msichana au mke kupewa idhini na baba yake kuolewa. Pia, iliwafanya wale wasioweza kuwa na uwezo kwa wakati huo kubaki makapera kwa muda mrefu wakiwa katika harakati za kutafuta mahari.

Mahari kamili ilikuwa ng'ombe kumi na wawili ambayo ndiyo ilikuwa shukrani kubwa kwa wazazi wa msichana. Hali hii ilifanya ng'ombe kuthaminiwa sawa na ufugaji. Utajiri uliambatanishawa na idadi kubwa ya mifugo. Watu walioana katika umri mkubwa.

Wasichana wengi walikuwa bikira au wanawali. Bikira alithaminiwa maana ilikuwa fahari kwa wazazi. Wazazi wa bikira walipewa zawadi pamoja na bikira kwa kubaki bikira au kujitunza. Zawadi hii ilikuwa mbali na mahari iliyolipwa.

Kujifungua nje ya ndoa miongoni mwa wasichana ilikuwa jambo la aibu sana kwa upande wa msichana mwenyewe na wazazi wake. Ikiwa hali ingetokea hivyo msichana aliozwa kwa lazima kwa mzee tajiri kama mke wake wa pili au hata wa tatu. Hata hivyo haikuwa hatia kama mvulana alipata mtoto nje ya ndoa au kabla ya kuoa rasmi.

Iwapo msichana alitoroka kwao na kuolewa, hilo halikutambuliwa hususan mume alikuwa hana mifugo au ng'ombe wa kulipa mahari. Mume mwingine ambaye alikuwa na mahari kamili angeweza kumuoa msichana kama huyo na hao watoto wengine aliokuwa amewapata na yule mume mwingine kumtambua kama baba yao. Ikiwa mume alikuwa na watoto nje ya ndoa na hakutaka kumuoa mama yao angelipa ng'ombe wanne kwa mtoto wa kiume na ng'ombe watatu kwa msichana. Mifugo hawa walipewa wazazi wa msichana aliyejifungulia kwao. Kiutamaduni, mume aliheshimiwa na wakwe zake pamoja na mkewe kutokana na umuhimu wa asasi ya ndoa na mahari aliyolipiwa. Mume au mke aliyebaki bila kuoa au kuolewa alifananishwa na mtoto, hakuheshimiwa hata kidogo. Hakupewa wadhifa wowote katika jamii.

Katika mauko au matanga ya mtu mzima ambaye hakuwa ameolewa au kuoa yalikuwa mafupi. Yaani ibada iliendeshwa kwa muda mchache na hapakuwa na mengi ya kuzungumuzwa. Isitoshe, hayakuwa na mbwembwe za aina yeyote ile katika aina hiyo ya mazishi. Msichana aliyeaga kabla ya kuolewa na ilhali alikuwa amekomaa alizikwa nje ya boma lao. Wageni kutoka upande wa mke, walipomtembelea binti wao walitarajia mapokezi murwa kutoka kwa mke wao. Mapokezi yao yalitegemea sana heshima ya mke kwa mume. Endapo mke alikuwa na madharau kwa mumewe hangetarajia mumewe kuwakaribisha wa kwao vyema. Ingawa hangewafukuza, hakuchangia katika mahitaji muhimu ya kuwalaki wageni. Ikumbukwe kuwa nyakati hizo kila mali bomani ilikuwa ya mume hata mke alichukuliwa kuwa mali ya mume wake. Mke hakuwa na mamlaka ya kumiliki mali yeyote hata watoto hawakuwa wake. Ili kurekebisha hali hii ya mapokezi duni kutoka kwa mumewe ilibidi mke abadili mienendo yake kwa mume wake. Yaani amuheshimu mumewe na amtambue kama kichwa cha nyumba.

Mke alipohitaji kuwatembelea jamaa zake aliomba ruhusa kutoka kwa mumewe. Akiwa kwao, mke alikuwa huru kutangamana na watu wa ukoo wake lakini kwa kuzingatia tamaduni za alipoolewa si za kwao. Mtazamo wa jamii kuhusu utamaduni ni kuwa tamaduni mbaya zilizopitwa na wakati zinafaa kutupiliwa mbali na nzuri zenye manufaa kudumishwa. Mathalan ulipaji wa mahari ulikuwa muhimu na kitambulisho mwafaka kwa jamii ya Wanyore. Kwa hali hiyo, ni jukumu ya wazee kuwafunza watoto ili utamaduni uweze kuendelezwa.

Hata baada ya maridhiano na msamaha na hali ya kurudia ya kawaida, Maadui wa awali wangekutumia salamu kuwapumbaza, salamu haimaanishi uhasama haupo. Jamii ya Wanyore ya Abaluhya haikuwa chokozi ilivyokuwa kwa jamii zingine. Vijana walifuzwa kutotumika uchokozi na kuwa tayari kutetea jamii kwa kila hali. Falsafa ya jamii ni kuwa uadui huweza kuchipuka ghafla licha ya maisha kuonekana ya kawaida. Ikitokea hivyo

lazima wajitetee, wawe tayari kuitetea jamii zao wakati wowote ikilazimu.

## Hitimisho

Methali za Wanyore zinaendeleza falsafa kupitia miktadha mbalimbali ya kijamii. Kupitia kwazo utamaduni na mila za kijamii zimejengeka na kuhifadhiwa ndani yake. Ufafanuzi wa methali umejikita katika tajriba za wanajamii na shughuli za kila siku za maisha yao kwa hivyo huhusisha masuala ambayo ni mwonoulimwengu wao. Hii inatokana na hali kwamba zimetokana na mazingira halisi na hivyo hutumiwa kuwasilisha masuala yote katika jamii. Kutokana na hali hii inabainika kwamba methali ni fasihi hai inayoendeleza shughuli za maisha katika jamii ya Wanyore na hivyo basi itaendelea kutekeleza wajibu huo hata siku za usoni.

Ingawa makala haya yamezingatia falsafa ya jazanda katika methali za Wanyore kwa mtazamo wa kisemantiki, imedhihirika kwamba mwonoulimwengu wa jamii ya Wanyore umejikita katika jazanda. Kwa hivyo ni kupitia jazanda hizi kumejengeka falsafa mbalimbali za wanajamii wa Wanyore. Ni kutokana na falsafa hizi jamii ya Wanyore ina mila na utamaduni wake wa kipekee unaorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ni uzito wa falsafa hizi umejenga utangamano na mshikamano wa kijamii kiasi kuwa kila mmoja huhisi kuwa ni sehemu ya jamii pana. Falsafa hizi vilevile zimedumisha jamii kiasi kwamba huleta hutoa mwongozo wa maisha ya kijamii ambao kila mmoja hujionea fahari na ni kitambulisho cha wanajamii. Kwa hivyo, mustakabali wa falsafa katika jamii ya Wanyore una thamani isiyomithilika na unazidi kupanuka na kujitanua zaidi. Ili kuendelea kukuza falsafa ipo haja ya kufanya utafiti na kuchapisha falsafa hizi kwa minajili ya kuzihifadhi katika maandishi na kufanya utafiti zaidi kuchunguza maana ya itikadi ya Kinyore na semi nyingine za kitamathali kwa kutumia usasa wa mabadiliko ya kiteknolojia katika lugha ya Kinyore na athari zake kwa utamaduni wa kijamii.

**Funding:** This research received no external funding.

**Conflicts of Interest:** The authors declare no conflict of interest.

**Disclaimer Statement**

This paper uses data from a thesis submitted to Masinde Muliro University of Science and Technology, Department of Language and Literature Education for award of a PhD degree. Title of the thesis: Falsafa ya Jazanda Katika Methali za Wanyore; Mtazamo wa Kisemantiki. Name of the supervisors: Dr Susan Chebet Choge and Dr Fred Wanjala Simiyu.

**Author Bionote**

Henry F. Andele is an Education Officer, before this, he had served as a teacher of Kiswahili for 19 years of which 6 years was as a part time lecturer at Masinde Muliro University of Science and Technology. He has a Bed Arts from Egerton University (2002), Med Kiswahili at Masinde Muliro University of Science and Technology (2015) and currently pursuing PhD in Linguistics Kiswahili at Masinde Muliro University iof Science and Techology. His areas of teaching expertise and research interest are; Linguistic in Kiswahili, Literature in Kiswahili and Comparative Linguistic in Kiswahili and other Afican Languages.

Susan Chebet-Choge is a Senior Lecturer and a Head of Languages, Linguistics, Literature and Common Undergraduate Courses at Koitaleel Samoei University (A Constitutent College of Nairobi University). Before this, she had served at Masinde Muliro University of Science and Technology as a Senior Lecturer of Kiswahili and Chairperson of Languages and Literature Education Department. She has a PhD in Educational Communication Technology (Kiswahili Education Option) from Moi University. Her areas of teaching expertise and research interest are educational linguistics (with special reference to Kiswahili education), pure linguistics, sociolinguistics, contact linguistics, onomastics, second language learning and language localization. She has supervised masters and PhD students to completion.

Fred Wanjala Simiyu holds a PhD in Kiswahili Studies with a bias in Comparative African Orality from Kenyatta University-Kenya. Currently, he a Senior Lecturer in the Department of Kiswahili and Other African Languages at Kibabii University, Bungoma - Kenya. Before joining Kibabii University, he worked as a lecturer at Egerton University (Kenya) and St. Augustine University of Tanzania. He has carried out research, taught and published widely in African Orality, Culture and Verbal Art.

**Marejeleo**

Chacha, C.N. (1987). Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Portrayal of Changing Society. Tasnifu ya Uzamifu (Ph.D.) Isiyochapishwa. Yale: Chuo Kikuu cha Yale.

Culler, J. (2001). The Pursuit of Signs: Semiotics, Literature, Deconstruction. New York: Routledge.

Imbosa, R. (1990). Jazanda Katika Ushairi wa Muyaka. Tasnifu ya Uzamili (M.A.) Isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Maitaria, J.N. (2012). Uanishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali. Tasnifu ya Uzamifu (PhD.) Isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Maitaria, J.N. (1991). Matumizi ya Methali kama Chombo cha Mawasiliano: Mtazamo wa Kiisimujamii. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Maitaria, J.N. na Momanyi, C. (2016). Visawe katika Methali Tafsiriwa za Kiswahili. Katika Jilala, H. (mh.). Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi. Dar es Salaam: Daud Publishing Company. Kur. 279-293.

Sperber, D. na Wilson, D. (1995). Relevance: Communication and Cognitive. Oxford: Blackwell.

Sperber, D. na Wilson, D. (2012). Pragmantics. Katika Wilson na Sperber Kur. 1-27.